



LIDA Stories

lidastories.net

Kuja Norwei / Venir en Norvège

✎ Aamiina

👤 Julie Cornelia van Walsum

👤 Jacob Haule (sw), Zina (fr)



This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

<https://creativecommons.org/licenses/by/4.0>

Kuja Norwei

Venir en Norvège



✎ Aamiina

👤 Julie Cornelia van Walsum

👤 Jacob Haule

📄 5

🗣️ KiswaHili / français



Mimi na kaka zangu wawili tulikuja Norwei mwezi Disemba 2016. Tulivaa nguo za majira ya joto kwa sababu tulifikiri Norwei kutakuwa na joto kama Somalia. Hata hivyo, tulipofika uwanja wa ndege kulikuwa na theluji. Tulihisi baridi na hali ya hewa ilikuwa ya baridi sana. Ingawa tulibeba mabegi, yalikuwa na nguo za majira ya joto tu.

...

Mes deux frères et moi sommes venus en Norvège en décembre 2016. Nous portions des vêtements d'été parce que nous pensions qu'il ferait aussi chaud en Norvège qu'en Somalie. Seulement, lorsque nous sommes arrivés à l'aéroport, il neigeait. Nous avons froid, et la météo était glaciale. Même si nous avons ramené quelques valises, elles ne contenaient que des vêtements d'été.

Même s'il faisait froid, j'étais très heureuse quand nous sommes venus en Norvège. Je pourrais enfin revoir ma maman, que je n'avais pas revu depuis six ans. Ma maman et deux de ses amies nous ont rencontrés. Quand nous l'avons vue, nous avons pleuré de joie. Nous sommes allés en voiture jusqu'à la petite ville où vit maman.

...

Hata kama kulikuwa na baridi, nilifurahi sana tulipokuja Norwei. Hatimaye niliweza kufanikiwa kuonana tena na mama yangu ambaye sikumuona kwa miaka sita. Tulionana na mama pamoja na rafiki zake wawili. Tulipomuona tulliia kwa furaha. Tulienda kwenye mji mdogo ambapo mama anaishi.





Siku za mwanzo tukiwa katika mji wa mama zilikuwa ni za kustaajabisha. Kulikuwa na baridi na theluji na hatukuweza kuona chochote. Mitaa ilikuwa tupu kabisa. Watu wachache niliokutana nao walionekana wakihihi baridi na hawakuwa sawa. Somalia kulikuwa na watu kila mahali, kwa hiyo kila kitu kilikuwa kigeni hapa. Mama yangu na rafiki zake walitupatia zawadi na kisha akatupeleka kununua nguo za majira ya baridi.

...

Les premiers jours dans la ville de maman étaient très étranges. Il faisait froid et il neigeait et il n'y avait pas grand chose à voir. Les rues étaient complètement vides. Les quelques personnes que j'avais rencontrées semblaient froides et antipathiques. En Somalie il y avait des gens partout, donc tout était inhabituel ici. Ma maman et ses amies nous ont offert des cadeaux, et après elle nous a emmenés acheter des vêtements d'hiver.



Kama ningebaki Somalia, ninadhani ningekuwa mama mpaka sasa. Pengine ningekuwa na watoto wengi. Kama ningekuwa Somalia, nisingekuwa na fursa sawa kama nilizozipata mpaka sasa. Ninajihisi mwenye bahati kuishi Norwei.

...

Si j'étais restée en Somalie, je pense que j'aurais été une mère à présent. Peut-être que j'aurais déjà beaucoup d'enfants. Si j'avais été en Somalie, je n'aurais pas eu les mêmes opportunités que j'ai maintenant. Je me sens chanceuse de vivre en Norvège.

Après les vacances de Noël, j'ai commencé une formation de Norvégien au centre d'éducation pour adultes. J'y ai étudié pendant deux ans avant de commencer dans une école normale. Je suis maintenant en dernière année, et je me suis fait plein de nouveaux amis. Je suis très sociable et j'aime rencontrer de nouvelles personnes.

...

Baada ya mapumziko ya Krismasi, nilijiunga na kozi ya kinorwei katika kituo cha elimu ya watu wazima. Nilisoma pale kwa muda wa miaka miwili kabla ya kuanza shule ya msingi. Sasa nipo mwaka wa mwisho na nimejitengenezea marafiki wengi. Ninapenda sana kuongea na watu na kufurahia kuonana na watu wapya.



L'année prochaine je vais rentrer au lycée dans la section de la santé et du développement de la jeunesse. À l'avenir, je veux devenir travailleuse sociale. Quand j'aurai terminé mes études, mon rêve est d'avoir un travail permanent. Je veux aussi apprendre à conduire et avoir mon permis de conduire.

...

Mwaka ujao, nitaanza shule ya sekondari katika idara ya afya na maendeleo ya vijana. Hapo baadaye, ninataka kuwatumikia vijana. Nikimaliza elimu yangu, ndoto yangu ni kupata ajira ya kudumu. Pia ninataka kujifunza udereva na nipate leseni yangu ya udereva.





Baada ya masomo, huwa ninaenda kwenye kituo kinachoendeshwa na wajitoleaji ambapo huwa ninasaidiwa kufanya kazi ya nyumbani. Pia nimejiunga na kozi ya kushona katika kituo hiki.

...

Après les cours, je vais dans un centre tenu par des volontaires où je me fais aider pour mes devoirs. Je me suis aussi inscrite dans des cours de couture dans ce centre.



Nilipokuwa Somalia, sikuwahi kwenda shule au kujiunga na kozi yoyote isipokuwa shule ya Kuran. Sikujua kusoma wala kuandika. Sasa nimeshajifunza namna ya kuandika Kisomali na Kinorwei na masomo mengine mengi. Bila elimu, nilijihisi si kitu. Sasa ninajiona mwenye maarifa na furaha.

...

En Somalie je n'étais jamais allée à l'école et je n'ai jamais suivi de formations, sauf pour l'école Coranique. Je ne savais ni lire ni écrire. Maintenant j'ai appris à écrire à la fois en Somali et en Norvégien, et plein d'autres matières. Sans éducation, j'avais l'impression d'être personne. Maintenant je me sens instruite et heureuse.